

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya



Simu. Na. 220 2325/2261
Fax Na. 220 2472
E-mail: ded@lindidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
306 Barabara ya Masasi,
S. L. P. 328,
65183 MTAMA-LINDI.

Kumb. Na. MDC/M.13/45/VOL.V/37

26/06/2023

TANGAZO LA KAZI YA MUDA MFUPI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama anapenda kuwatangazia wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama na nje ya Mtama kuwa anatangaza nafasi za kazi za muda mfupi katika uendeshaji wa Mgahawa wa Halmashauri kwa mtu mwenye sifa zilizoainishwa katika kila nafasi kama ifuatavyo:-

1: Meneja wa Mgahawa nafasi 01

Sifa zinazotakiwa:

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe na Eimu ya Sekondari kidato cha nne au sita na mwenye Astashahada (cheti) au Diploma (Stashahada) katika fani ya:-
 - Usimamizi wa hoteli
 - Usimamizi wa Biashara
 - Usimamizi wa fedha
 - Utawala
- iii. Awe na umri usiozidi miaka 45

2: Wahudumu wa mgahawa/hoteli – Nafasi 04

Sifa zinazotakiwa:

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 45

- iii. Awe na Elimu ya Kidato cha nne au cha sita
- iv. Waombaji wa nafasi hii wenye cheti cha Usimamizi wa Hoteli watapewa kipaumbele zaidi

3: Wapishi wa Mgahawa/Hoteli – Nafasi 03

Sifa zinazotakiwa:


- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha nne au cha sita
- iii. Awe na umri usiozidi miaka 45
- iv. Waombaji wa nafasi hii wenye cheti cha fani ya upishi au usimamizi wa jiko na hoteli watapewa kipaumbele zaidi

Mambo muhimu ya kuzingatia:

- Waombaji wote waambatishe maombi yao na vivuli vya vyeti vya taaluma na ujuzi
- Waombaji waambatishe maombi yao na utambulisho kutoka katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji au Kata
- Waombaji waweke picha mbili (02) za passport size
- Waombaji waonyeshe anuani zao halisi
- Mwisho wa kupokea maombi itakuwa tarehe 10/07/2023 saa 9.30 Alasiri
- Maombi yote yaandikwe kwa Mkono na kuwasilishwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mtama,
306 Barabara ya Masasi,
S. L. P. 328,
65183 MTAMA-LINDI.

Tangazo hili limetolewa na,



George E. Mbilinyi,
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya – Mtama.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MTAMA